

HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA

TAARIFA YA UJENZI KITUO CHA AFYA MIMA

Halmashauri ya wilaya ya Mpwapwa imepokea kiasi cha Shilingi milioni **500,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya Mima. Ujenzi huu unafanyika kwa kutumia teknolojia ya Pre-fabricated materials kwa kumtumia Mkandarasi ambaye ni Global Space East Africa.

MAJENGO YANAYOJENGWA KATIKA KITUO HIKI NI:-

1. Jengo la Upasuaji (Theatre)- Thamani yake ni **153,520,151/=**
2. Nyumba ya mtumishi (Staff Quarters)- Thamani yake ni **90,094,822/=**
3. Maabara (Laboratory)- Thamani yake ni **140,314,975/=**
4. Wodi ya watoto (Childrens Ward)- Thamani yake ni **53,933,581/=**
5. Wodi ya Kina mama (Maternity & Delivery)- Thamani yake ni **62,136,122/=**
Jumla kuu ikiwa na thamani ya shilingi **499,999,650/=**
Ujenzi wa majengo mengine ambayo yapo katika mkataba ya ziada ni;-
6. Kichomea taka (ReadyMade Incinerator)
7. Jengo la kuhifadhi maiti (Mortuary)

HATUA YA UJENZI ILIYOFIKIWA

Majengo matano ujenzi wake umeanza, ambayo ni Jengo la Upasuaji, Jengo la nyumba ya mtumishi, Maabara, Wodi ya watoto na Wodi ya akina mama, Misingi imechimbwa, zege ya chini (blinding) imewekwa na misingi imejengwa, zege la msingi limewekwa katika misingi ya majengo matatu, vifaa vya ujenzi vipo eneo la ujenzi ikiwemo prefabricated materials.

Zifuatazo ni picha za ujenzi huo

Jengo lililopo ambalo litatumika kama OPD



Ujenzi wa msingi ukiendelea



Ujenzi ukiendelea



VIFAA (MATERIALS) MBALIMBALI VIKIWA SITE

Roof



Tofali







MAFANIKIO

1. Kazi imeanza na inaendelea vizuri.
2. Eneo lote la kituo limefanyiwa uhakiki wa mipaka.
3. Ujenzi wa kituo hiki unakadiriwa kumalizika mwanzoni mwa mwezi Januari 2018.